


**TAMKO LA CHAMA CHA WANASHERIA TANGANYIKA
KANDA YA BAGAMOYO DHIDI YA KAULI YA MKUU WA
MKOA:**

Kanda ya Bagamoyo inaundwa na mawakili wa wilaya za Kinondoni, Ubungo na wa mkoa wa Pwani. Hivyo wilaya za Kinondoni na Ubungo ni sehemu ya Mkoa wa Dar es Salaam. Tumesikitishwa na kauli ya mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliyoitoa hivi karibuni na ambayo imekuwa ikisambaa katika mitandao ya kijamii akielekeza kuwa “kibaka atakayekamatwa apelekwe maabara ili awe chombo/skeleton ya kufundishia kwa wanafunzi wanaotaka kuja kuwa wezi”.

Ni kweli wizi ni mbaya sana lakini jamii yetu ya watanzania hatupaswi kufika huko alikoagiza Mkuu wa mkoa. Tukiruhusu kujichukulia sheria mkononi kama alivyoelekeza Mkuu wa mkoa hii nchi itakuwa haiheshimu mfumo wetu tuliojiwekea wa utoaji haki na ni kauli hii ya Mkuu wa mkoa ni ya hatari kwa amani na utulivu uliopo nchini.

Kauli hii ya Mkuu wa mkoa inakwenda kinyume na Katiba ya Jumhuri ya Muungano ya Tanzania ambayo imetoa haki ya kuishi. Ni rai yetu kwa viongozi wote wa umma ambao wameapa kuulinda Katiba kufanya hivyo. Kwa mujibu wa sheria chombo pekee chenye mamlaka ya kuwatia hatia watuhumiwa wa makosa ya jinai ni mahakama na sio viinginevyo na hivyo maelekezo ya kuwafanya watuhumiwa kuwa chombo/skeleton ya kufundishia maabara ni ya hatari kwa ustawi wa Taifa letu.

Kutokana na ukweli kuwa kauli kama hizi zinazokwenda kinyume na Katiba na Sheria zetu zimekuwa zikitolewa na Mkuu huyu wa mkoa mara kwa mara, ni rai yetu kwa Mkuu wa Mkoa kufanya yafuatayo:



1. Kwanza Mkuu wa mkoa atoke hadharani na kufuta kauli hiyo ambayo inaweza kufanyiwa kazi na wasaidizi wake kama polisi nk. na kuleta maafa kwa wananchi ambao bado hawajatiwa hatiani.
2. Pili Mkuu wa mkoa ahimise wasaidizi wake kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wote wa uhalifu kama sheria inavyoelekeza.
3. Tatu tunamsihi Mkuu wa mkoa ambae mara kwa mara amekuwa akitoa kauli tata na zinazokinzana na Katiba na Sheria kuzingatia Katiba na Sheria kila mara anapotoa maagizo yake. Chama cha wanasheria Tanganyika tupo tayari wakati wowote kumpa msaada wa kisheria kabla hajatoa maagizo ambayo hana uhakika kama yanapingana na Katiba au Sheria.
4. Nne ikiwa Mkuu wa mkoa hatafuta kauli yake hiyo tunakusudia kufikisha suala hili mahakamani ili kulinda haki ya kuishi.

Mwisho Chama cha Wanasheria Tanganyika Kanda ya Bagamoyo kitaendelea kupinga kauli zote zinazotweza utu wa mwanadamu, kauli zote zinazokwenda kinyume na Katiba na Sheria zetu, kauli zote zinazokwenda kinyume na Haki za binadamu ambazo zitatolewa na kiongozi au mtu yeyote.

Tunawaomba Wanzania wote kutokubali kuvunja Katiba na pia kutokubali kuvunja Sheria za nchi kwani kufanya hivyo atakaewajibika mbele ya mahakama ni mvunja Sheria na sio kiongozi aliempa maelekezo.

REGINALD SHIRIMA
MJUMBE WA BARAZA LA UONGOZI NA KIONGOZI WA
CHAMA CHA WANASHERIA WA TANGANYIKA KANDA
YA BAGAMOYO

20/01/2025